

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

**Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir/Wilaya ya Sudan Wakutana na Mwenyekiti wa Chama cha Muungano wa Wanachi (UPF) (Imetafsiriwa)**

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir, ulioongozwa na Ustadh Nasir Ridha, Mkuu wa Kamati Kuu ya Mawasiliano ya Hizb ut Tahrir / Wilayah ya Sudan, na mwanachama Ustadh Montasir Karrar, Mratibu wa Amali za Kamati ya Mawasiliano katika mji wa Gadharef, na Ustadh Muhammad Mukhtar, Mwanachama wa Hizb ut Tahrir, walikutana na Al-Amin Daoud, Mwenyekiti wa Chama cha Muungano wa Wanachi mjini Port Sudan, Ijumaa, 24 Shawwal 1445 H sawia na 3/5/2024 M.

Mgogoro wa Sudan, vita vinavyoendelea na matokeo yake yalijadiliwa. Pande zote mbili zilisisitiza umuhimu wa suluhisho kuwa mbali na uingiliaji kati na ajenda za kutoka nje, na kwamba suluhisho lazima litokane na itikadi tukufu ya Uislamu, haswa kwa vile migogoro ya kikabila na kieneo imesababisha hali ya usalama, kisiasa na kiuchumi kuwa ngumu, na inaweza kuvuruga. Nchi. Hakuna kitu kinachowaunganisha watu wote wa Sudan isipokuwa itikadi tukufu ya Uislamu, inayotukuza thamani ya udugu wa Kiislamu.

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)  
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir  
katika Wilayah Sudan**